# OPENER STD 7 TERM 2 2020
# KISWAHILI

NAME…………………………………………………………………………………………

Learner's Number [ ][ ][ ]

Gender Boy [ ] Girl [ ]

County name ………………………………………… County code [ ][ ][ ]

Sub county name ………………………………………… Sub county code [ ][ ][ ]

School name ………………………………………… School code [ ][ ][ ]

The grid below is to be filled by the teacher after marking the learner's work

| | Level 1 | Level 2 | Level 3 | Level 4 |
|---|---|---|---|---|
| Numbers 1-15 | | | | |
| Measurement 16-23 | | | | |
| Geometry 24-25 | | | | |

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1-15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Mchezo wa riadha ni __1__ ya michezo __2__ zaidi nchini. Taifa la Kenya __3__ kote ulimwenguni __4__ kukuza wanaspoti mahiri. Kila mwaka __5__ wa Kenya __6__ beramu __7__ Kenya nchi za nje. Wanaspoti hawa hupewa heshima kuu. Ndiposa wahenga walisema __8__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. moja | B. mojawapo | C. mmojawapo | D. mmojazipo |
| **2.** | A. nzuri | B. mibaya | C. almaarufu | D. maarufu |
| **3.** | A. yamesifika | B. imesifika | C. limesifika | D. wamesifika |
| **4.** | A. katika | B. kama | C. bali | D. mradi |
| **5.** | A. wanasoka | B. wanaraga | C. wanariadha | D. wanajeshi |
| **6.** | A. wanapeperusha | B. hupeperusha | C. tulipeperushiwa | D. hushusha |
| **7.** | A. ya | B. la | C. wa | D. za |
| **8.** | A. asiyesikia la mkuu huvunjika guu | B. usipoziba ufa utajenga ukuta | C. kidole kimoja hakivunji chawa | D. chanda chema huvikwa pete |

Mwendo __9__ saa tano usiku, nilisikia mbisho hafifu mlangoni. Mtu huyo aliniomba __10__ aingie chumbani __11__ kujikinga __12__ mvua kali. Nilipomfungulia __13__ macho hapa na pale kama mtalii. Kumbe mgeni wangu hakulala __14__. Aliponisikia __15__ usingizini, aliiba mali yetu iliyokuwa sebuleni.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | A. ya | B. wa | C. la | D. za |
| **10.** | A. nimkataze | B. aniruhusu | C. nimruhusu | D. niwaruhusu |
| **11.** | A. yake | B. chake | C. lake | D. mwangu |
| **12.** | A. dhidi ya | B. baina ya | C. kati ya | D. chini ya |
| **13.** | A. alipiga piga | B. alikimbia kimbia | C. aliangaza angaza | D. alifumba fumba |
| **14.** | A. ? | B. ! | C. , | D. . |
| **15.** | A. nikilia | B. nikinguruma | C. niking'orota | D. nikikoroma |

*Kutoka swali la* **16** *mpaka* **30**, *chagua jibu sahihi.*

**16.** Chagua neno ambalo haliambatani na kisawe chake.
A. sahibu - rafiki
B. rabuka - maulana
C. chakura - chakula
D. kibali - idhini

**17.** Mlango wa gari umejifunga wenyewe 'ji' imetumika kuonyesha
A. kirejeshi
B. mtendaji
C. hali
D. ukubwa

**18.** Mwanafunzi **mtiifu** anasoma ilhali **yule** mzembe hasomi. Maneno yaliyopigwa mstari ni
A. kuhusishi, kielezi
B. kivumishi, kiwakilishi
C. kivumishi, kielezi
D. kiwakilishi, kivumishi

**19.** Masaibu alimharibia nyonda mali yake. Mahakama ilimwagiza masaibu amlipe
A. faida
B. faini
C. fola
D. fidia

**20.** Tegua kitendawili hiki.
Hucheka wakati wote.
A. Ngiri
B. Ndege
C. Fisi
D. Radi

**21.** Chagua sentensi yenye kimilikishi cha nafasi ya tatu.
A. Gari lenu lilioshwa jana
B. Kuku wangu ameanza kutaga.
C. Maswali yao yalikuwa magumu.
D. Mswaki wako umechafuka.

**22.** Mtoto wa sungura huitwa
A. Shibli
B. Kiyoyo
C. Kinengwe
D. Kitungule

**23.** Mafuta, uji, moshi, unga na majini nomino za
A. jumla
B. wingi
C. dhahania
D. maalum

**24.** Chagua sentensi inayohusisha '**po**' ya wakati
A. Walipoketi wageni ni safi.
B. Painamapo ndipo painukapo.
C. Alipoenda kwake hakumkuta.
D. Po! Usije hapa na kelele zako.

**25.** Chagua sentensi yenye kielezi cha idadi.
A. Watoto walipumzika kidogo.
B. Safari yetu ilianza jana.
C. Wanafunzi walifika nyumbani mapema.
D. Tulijitolea kufa kupona kuishinda timu ile.

**26.** Nomino uwanja inapatikana katika ngeli ya
A. U - U
B. U - ZI
C. U - YA
D. U - I

**27.** Mfano wa kiashiria cha mbali kidogo ni
A. huo
B. hii
C. kile
D. hawa

**28.** Chagua hali ya kawaida ya sentensi hii.
Vijikapu vimejaa vitabu vyao.
A. Kikapu kimejaa vitabu vyao.
B. Kikapu kimejaa vitabu zao.
C. Vikapu vimejaa vitabu vyao.
D. Kikapu kimejaa kitabu chao.

**29.** Sahihisha: Shuleni kwao pana nyasi ndefu.
A. Shuleni pao kuna nyasi ndefu.
B. Shuleni yao ina nyasi ndefu.
C. Shuleni pao mna nyasi ndefu.
D. Shuleni kwao kuna nyasi ndefu.

**30.** Kanusha: Kula kwake kulimshibisha.
A. Kula kwake hakumshibishi.
B. Kutokula kwake hakumshibisha
C. Kutokula kwake hakukumshibisha.
D. Hakula wala kushiba kwake.

*Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali kuanzia* **31** *mpaka* **40**

Ebu sikiliza waraka wa mzee isemavyo. Radhia akamwambia mume wake.

"Wewe siku hizi umenisahau. Huniletei chochote wala kunitumia hela. Mama yako, dada yako na ndugu zako pia hawana chakula wala nguo. Watoto wa ndugu yako hawaendi shuleni kwa ukosefu wa karo. Endapo, mtoto hawezi kuwatunza wazazi wake ni faida gani ya kuzaa au kuzaliwa? Ikiwa huwezi kuwasaidia ndugu zako na watoto wao pia wapate elimu kama ulivyopata wewe basi faida ya kuwa ndugu, kaka, mjomba, baba mdogo au baba mkubwa wao ni upi? Ama kweli pale mwanzo ulipoanza kufanya kazi ulifanya juhudi kubwa kutimiza wajibu wako. Sasa mimi babako matumaini yangu ni nini? Radhi yangu na ya babu zako utaipataje ikiwa tabia yako ni hii?"

"Wasikia mke wangu lawama hizi zote zimeletwa na mitindo ambayo haiwezi kutuletea maendeleo," alisema Bwana Mbotela baada ya kusoma vifungu kadhaa vya waraka wa babake.

"Mama aliyenizaa ndiye aliyekuwa mkulima nyumbani kwetu. Baba hakupenda kufanya kazi yoyote. Wakati wa mchana alimngojea mama aende shambani akalime mpaka arudi kisha ampikie chakula ili aweze kwenda kutafuta pombe wakati wa adhuhuri. Asubuhi yote alimaliza kitandani au kuzurura katika nyumba za watu wengine **akipiga gumzo** na mabwana **wazembe** wenzake. Bila ya kujali kazi ngumu mama aliyokuwa akifanya, baba alisikika mara nyingine akimkaripia mama huku akimtolea cheche za matusi kwa sababu ya kuchelewesha chakula chake cha mchana."

"Mama Mbotela," alisema baba. "Chakula kiko wapi? Huu ni uvivu wa mwanamke au ni balaa? Huko shambani ulikuwa wafanya nini tangu asubuhi hata ukanichelewesha kwenda nikatafute pombe. Ugoigoi huu nitaukomesha! Nikikosa kupata mboko leo utakipata cha mtema kuni. Huwezi kumheshimu dume kama mimi?"

"Wakati wa matusi kama hayo alinyamaza kimya. Aliliondoa jembe lake kutoka kwenye bega lake la kulia na kuliingiza ndani ya nyumba. Halafu akaendelea na kazi yake ya kawaida ya kumtengenezea chakula mume wake mvivu kwa haraka ili asichelewe kwenda kushiriki ulevi."

"Hata hivyo mzee wangu hakuwa na huruma wala shukrani. Kila siku alipokosa pombe alimpiga mama bila huruma. Aidha, kila siku aliyolewa kupita kiasi alirudi nyumbani na kumfanyia mama ukatili zaidi. Basi haikuwa ajabu kamwe kwamba mama hakuishi miaka mingi. Mbali na maisha ya ukatili na utumwa katika nyumba yetu ya wavivu ilikuwa ni wajibu wake wa kunitafutia karo ya shule. Baba yangu hakukubali kabisa kujisumbua kwa njia yoyote ile ndio nisome. Mara nyingi alitafuta zile pesa za mama alizokuwa akichuma nikatoe karo ili akanunue pombe. Kuwavisha watu wote wa nyumbani na kutafuta karo yangu ulikuwa uzito mno kwa mama. Hata baada ya miezi miwili ya kwanza ya kazi yangu na ualimu, mama alifariki kwa ghafla kutokana na maradhi ya mkamba."

"Hapo ndipo jamaa zangu walijaribu kunibandika mzigo wa mama wakifikiri nitaendelea kuwapatia vitu vya bure milele na milele kwa sababu ya kuwa damu moja nao. Nilijaribu kufanya hivyo kwa muda mfupi, lakini nikaona wamekuwa makabila makubwa ambao walikuwa tayari kuninyonya damu kama kupe.

Basi nami nikawa sina budi kukataa maisha ya utumwa na nikauacha mtindo huo wa kuwapelekea wavivu, makabila, kupe, wanyonyaji vitu vya bwerere." Akaendelea Bwana Mbotela.

---

**31.** Barua iliyosomwa, iliandikiwa nani?
A. Bi. Mbotela
B. Bw.Mbotela
C. Mkwe wake
D. Mjomba wake

**32.** Mwenye kuandika barua hii ni rahisi sana mwisho wake asipate
A. radhi
B. faida
C. mke
D. mjomba

**33.** Kulingana na kifungu hiki, Bw.Mbotela alikuwa
A. mzembe
B. mchoyo
C. karimu
D. mwenye bidii

**34.** Baba yake Mbotela aliutumia muda wake mwingi kwa
A. kufanya kazi.
B. kulala mchana wote.
C. kutafuta pombe kila kuchao.
D. kumsaidia mkewe kufanya kazi.

**35.** Ni sentensi ipi inayoonyesha kuwa babake Mbotela hakujali kazi ngumu mkewe aliyokuwa akifanya?
A. "Huwezi kumheshimu dume kama mimi?"
B. "Huko shambani ulikuwa wafanya nini hata ukanichelewesha kuenda kutafuta pombe "
C. "Chakula kiko wapi? Huu uzembe wa mwanamke au ni balaa?"
D. "Nikikosa kupata mboko leo utakipata cha mtema kuni."

**36.** Sababu ya mamake Mbotela kumtengenezea mumewe Mbotela kumtengenezea mumewe chakula kwa haraka ilikuwa mumewe asichelewe kuenda
A. kupiga gumzo.
B. kutafuta pombe.
C. kushiriki ujenzi wa taifa.
D. kuenda kumtafutia bibiye chakula.

**37.** Baada ya kukaripiwa na mumewe, mama Mbotela
A. hakusema kitu.
B. alimkaripia pia.
C. alimtukana bwanake.
D. alilia kwi kwi kwi

**38.** Ni kweli kusema kuwa
A. Bi.Mbotela alisaidiwa.
B. Mbotela alimsaidia mkwewe.
C. Mbotela hakumsaidia mkwewe.
D. Bi.Mbotela alikuwa mvivu.

**39.** Mwandishi wa makala haya anasema kwamba mzigo mzito wa mamake ulikuwa
A. kulima, kupika na kuteka maji.
B. kuvumilia mateso na matusi.
C. kuwalisha, kuwavisha watu wote nyumbani.
D. kutafuta pesa za karo na kushiriki ulevi.

**40.** Mwandishi amewaita jamaa wake kupe. Hii ina maana kuwa
A. walikuwa wazembe.
B. walikuwa hawana kazi.
C. walikuwa wakinyonya damu yake.
D. walipenda kupewa vitu na kutumikiwa bila ya wao kufanya kazi.

*Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali* **41** *mpaka* **50**

Ukitaka kufaulu maishani lazima ujue kuwa una kazi kubwa sana inayokungoja. Baada ya kuikabili vilivyo kazi hiyo kwa kutumia nyanja mbalimbali utayaimarisha maisha yako.

Karibu kila mtu aliyestawi amepitia katika vikwazo vingi tena vya kutatiza ajabu kuliko vikwazo wanavyopata vijana wa kisasa. Vijana wote wanatakiwa sasa wasugue bongo zao sawasawa ili watende mambo mengi mazuri kuliko wanayoyaona. Wasitosheke na yale yaliyotendwa na wazee. Kila kijana iwapo atakuwa na moyo kama huo nchi zote zitaendelea kwa kasi.

Kwa kujisaidia katika kujiendeleza, yafuatayo yanafaa kuzingatiwa. Vijana wanatakiwa wawe watoto wenye kuelewana na wazazi wao ambao watawaelekeza vyema kitabia na wakiwa ni wazazi waelewa, watawapa watoto wao maelekezo na **radhi ambayo ni bora kuliko mali**. Watoto wenyewe wajue wanataka nini, wawe na malengo katika maisha yao na wakanie kupata kile wanachokitaka bila kukata tamaa, watie bidii sana. Wasipoteze wakati wao bora kwa kufanya mambo yasiyo na faida.

Wapende kusoma bila kulazimishwa kwani kulazimishwa hakusaidii chochote. Ni sawa na ng'ombe alazimishwaye kwenda kunywa maji lakini akifika mtoni akatae kunywa maji yale. Mtoto mwenyewe anatakiwa ajitafutie na ajue kuwa mtoto wa tamaa anayependa kupewa zawadi ama peremende kila saa. Lazima ajue kuwa kupewa na kutopewa yote ni sawa. Mtoto anatakiwa kuwa mwelewa sana. Anatakiwa awe na ile fikra ya kujitafutia. Hata kama anatoka katika hali ya utajiri, azidi kutafuta ili ikiwezekana atajirike hata zaidi. Asitegemee cha ndugu kwani huenda akafa akiwa maskini. Chako ni bora kuliko kikubwa cha mwenzio.

Vijana wanatakiwa kuwa na nidhamu ya kiwango cha juu popote pale walipo. Wawe ni watu wenye kujiamani, wasikate tamaa kwa ajili ya maneno ya wivu yanayosemwa na wengine. Wasikate tamaa wanapoyaona masomo ni magumu, wakazane kuyaelewa kwani mwisho wataelewa na kufanikiwa. Wasiwadharau walimu au wenzao, wasipoteze wakati wao kusengenya. Wawapuuze wanaowanyanyasa, hata neno moja la kuwaudhi wanaloambiwa na wenzao na kuwachukulia vizuri na wawaheshimu kwa vile walivyo.

Wasithamini vitu vya anasa sana kama mavazi ya kitajiri. Wengi wasio na chochote wanaopuuza mambo ya anasa ndio wanafaulu sana katika maisha. Wengi wenye jamaa hawafaulu hugeuka kuwa wezi na kuishia gerezani.

Kijana atende jambo lolote kwa uangalifu bila kuchanganya mambo mengi pamoja. Akumbuke kuwa mtaka yote kwa pupa hukosa yote. Kijana asiogope mashindano kwani mashindano huleta ufanisi.

Kama huumwi ya nini ulale saa mbili za usiku na kuamka saa nne asubuhi ambapo mtu mwingine analala saa tano usiku na kuamka saa kumi na moja za asubuhi? Bila shaka mtu wa pili ama anakesha kwa kutenda mambo ya kimaendeleo atafanikiwa sana na yule wa kwanza atarudi nyuma kimaendeleo.

41. Kulingana na aya ya kwanza mwandishi anasema ili ufaulu ni
A. sharti ujulikane na wengi.
B. sharti aende nyanja mbalimbali.
C. sharti ujue kuna changamoto tele.
D. ufanye kazi kwanza katika nyanja mbalimbali.

42. "Karibu kila mtu aliyestawi amepitia katika vikwazo vingine." Hii ina maana kuwa
A. inabidi uwe tayari kuwaza na kuwazua zaidi.
B. ilibidi ujifunge kibwebwe kutatua matatizo.
C. ategemee wenzake kufaulu maishani.
D. ajiepushe na vikwazo anayokumbana nayo.

43. Hatua ya kwanza ya kufaulu kwa vijana kulingana na kifungu hiki ni
A. waonyeshe nidhamu bora kwa jamii.
B. kutatua vikwazo vya wazazi wao.
C. kutumia teknolojia kufaulu maishani.
D. kuwahusisha wazazi wao kuwaelekeza.

44. Ni mambo gani hayatamsaindia kijana kufaulu maishani
A. kujiamini.
B. utovu wa nidhamu..
C. nidhamu ya hali ya juu.
D. wasikate tamaa.

45. Methali gani inalingana na:
Mtegemea cha ndugu huenda akafa maskini.
A. Akili ni mali.
B. Mwenda tezi na omo marenjeo ni ngamani.
C. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
D. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

46. Mwandishi amesema "radhi ambayo ni bora kuliko mali" Hii inamaanisha
A. ushauri nasaha ni bora kuliko mali.
B. vijana waridhike na utajiri wao.
C. mali bila maridhiano haifai.
D. radhi ni sawa na mali.

47. "**Ng'ombe alazimishwaye kwenda kunywa maji**" ni msemo unamrejelea
A. wanyama
B. wawekezaji
C. wazazi
D. vijana

48. Ili kujisaidia katika kujiendeleza mwandishi ametaja hoja ngapi?
A. nne
B. tano
C. sita
D. saba

49. Kifungu hiki kimetumia methali ngapi?
A. mbili
B. tatu
C. tano
D. nne

50. Ni methali gani isiyolenga kifungu hiki.
A. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.
B. Mtegemea cha nduguye hufa maskini.
C. Mtaka yote hukosa yote.
D. Mwangata mbili moja humponyoka.